

JINA.....NAMBA YAKO.....

JINA LA SHULE.....SAHIHI.....

102/3  
KISWAHILI  
KARATASI LA 3  
FASIHI  
JULAI/AGOSTI  
MUDA: SAA 2 ½

**MTIHANI WA MWIGO KAUNTI NDOGO YA KAKAMEGA KUSINI-2016**

*Hati ya Kuhitimu Masomo ya Sekondari – Kenya (K.C.S.E)*

102/3  
KISWAHILI  
KARATASI LA 3  
FASIHI

**MAAGIZO**

- a) Jibu maswali manne pekee.
- b) Swali la kwanza ni la lazima.
- c) Usijibu zaidi ya swali moja kutoka sehemu moja.
- d) Mtihani huu una jumla ya alama 80.

*Hii karatasi ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.  
Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote nne za karatasi hii ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na  
kuwa maswali yote yamo.*

## **SEHEMU YA A**

### **SWALI LA LAZIMA: FASIHI SIMULIZI**

1. i) Tofautisha vipera vifuatavyo vya fasihi simulizi (al.4)
  - a) Ngoma na ngomezi
  - b) Mighani na ngano za mashujaa
- ii) Taja aina nne za ngomezi kwa kipindi cha sasa. (al.2)
- iii) Fafanua sifa nne za mlumbi. (al.4)
- iv) Linganua vitendawili na methali (al.8)
- v) Andika sifa mbili za maapizo. (al.2)

## **SEHEMU YA B**

### **KIDAGAA KIMEMWOZEA**

2. Riwaya ya kidagaa imeangazia maudhui ya utengano. Thibitisha. (al.20)

**AU**

3. “Mimi si mwerevu sana lakini pia si mjinga wa mwisho.”
  - a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)
  - b) Eleza sifa za msemaji (al.6)
  - c) Mzungumziwa anaendeleza maudhui ya usiri. Thibitisha. (al.10)

## **SEHEMU YA C: MSTAHIKI MEYA**

4. “Haina haja kuniondoa. Ungeniambia kuondoka ningeondoka tu.”
  - a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (al.4)
  - b) Fafanua sifa zozote nne za msemaji. (al.8)
  - c) Toa ithibati kuwa nchi ya cheneo imejaa ufiadi. (al.8)

**Au**

5. Jadili jinsi maudhui ya usaliti yanavyofafanuliwa katika tamthilia ya mstahiki Meya. (al.20)

**6. SEHEMU YA D: USHAIRI**

**(al.20)**

**SIGOMBE KIVULIE**

Ndege akiwa angani ,usiseme wangu mie  
Mngoje atue chini, na ndipo mgombanie  
Lakini yupo hewani,tama isikwingie  
Sigombeee kivulie,ndege apaa angani.

Ndege apaa angani,sigombeee kivulie  
Manapigana machoni, mwagombea uzurie  
Mwalizana kama nyani,matunda mwagombeee  
Sigombeee kivulie,ndege apaa angani.

Shika awe mkononi,ndipo ukajivunie  
Umshikapo mwilini,chukua kajifugie  
Kama utavyo moyoni,kufuga kajifugie  
Kama utavyo moyoni,kufuga ama mwachie  
Sigombeee kivulie,ndege apaa angani.

Usimlilie nyuni,kwanza akukaribie  
Na sauti mdomoni,aimbapo usifie  
Saburi ndicho kiini,kila jambo sivamie  
Sigombeee kivulie,ndege apaa angani.

Mwaingia ushindani,kwa magumu mpanie  
Ninyi nyote ufukani,ndege juu muanie  
Ndege ataturalini?, pengine ajiendee  
Sigombeee kivulie,ndege apaa angani.

Siingie ujingani,majambo mfikirie  
Sirukie kifanani,ndege juu muanie  
Utafanywa hayawani,jirani wakubeue  
Sigombeee kivulie,ndege apaa angani.

Atuapo matawini,kwa jicho kuangalie  
Awaone dharauni,na mbawa awapigie  
Na mate yamo kinywani,katu asiwasogee  
Sigombeee kivulie,ndege apaa angani.

Kaditama upigani,akheri amuambae  
Wawindaji pendaneni,mwachie ndege apae  
Lisha aliye tunduni,wa juu sitegemee  
Sigombeee kivulie,ndege apaa angani.

***Maswali***

- (a) Eleza dhamira ya shairi hili (al.2)
- (b) Taja na utoe mifano ya mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi hili (al.4)
- (c) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari (al.4)
- (d) Eleza jinsi uhuru wa mtunzi unavyojitokeza katika shairi. Tolea mifano jibu lako (al.4)
- (e) Eleza umbo/muundo wa shairi hili (al.4)
- (f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi (al.2)
- (i) Nyuni
- (ii) Wakabue

**SEHEMU YA E: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

7. Msiba unaowapata wanawake katika diwani hii ni wa kujitakia. Thibitisha kwa kurejelea wahusika wafuatao;
- a) Jamila (al.4)
- b) Sela (al.4)
- c) Christine (al.4)
- d) Lucy (al.4)
- e) Kudura (al.4)